



Kujifunza nyumbani

Bango hili ni kwa ajili ya nani?

- Ni kwa **familia zote** za watoto wenye ulemavu na wasio na ulemavu.
- Ni kwa **kila mtu** - mama na baba, walezi, watoto, ndugu, bibi na babu, mjomba na shangazi....

Je, bango hili linahusu nini?

Inaweza kuwa ni wakati mgumu skuli zimefungwa na watoto wako nyumbani. Unataka kuwasaidia watoto wako kujifunza kama ambavyo hufanya wakiwa skuli, lakini hii sio rahisi.

Bango hili linaonesha njia nyingi ambazo familia huwa wanazitumia kujifunza nyumbani. Mtu yeyote anaweza kutumia maoni yake mwenyewe na ubunifu kuongezea kwenye njia hizi za kujifunzia.

Ni kwa nini bango hili lilitayarishwa?

Bango hili linazisaidia familia kuwa na uwelewa zaidi kuhusu **namna kujifunza kunavyofanyika nyumbani** na namna kujifunza nyumbani kunavyoweza kusaidia kuimarisha kujifunza katika skuli na katika jamii.

Ni vipi utalitumia bango hili?

- Liweke kwenye ukuta wako ambapo kila mtu katika familia anaweza kuliona. Washirikishe watoto wako kuamua mahali pa kuliweka.
- Liangalie bango hili wakati wowote.
- Fikiria juu ya picha zilizomo katika bango. Je, picha gani unaipenda kuitazama zaidi?
- Unaona nini? Je, unafikiria nini kinachotoka kwenye picha?
- Je, linakupa maoni gani ya kujifunza nyumbani?
- Hakuna majibu sahihi au yasiyo sahihi.

Vitu rya kukumbuka wakati wa kujifunza nyumbani

Kujifunza hufanyika kila wakati tunaposikilizana na tunaposilikiliza mazingira yanayotuzunguka ...

- Kila mmoja husikiliza. Watu wazima husikiliza watoto, watoto husikiliza watu wazima, watu wazima husikiliza watu wazima na watoto husikiliza watoto.
- Omba msaada unapokuwa huelewi kitu fulani. Mtu yeyote anaweza kusaidia.
- Simulia hadithi ukitumia ishara na ishara za uso. Hakikisha kila mtu anaweza kukuona wakati unasililia hadithi.
- Sikiliza vilivyo karibu na wewe - ndege, wanyama, mvua. Jaribu kutengeneza sauti zinazofanana. Kujifunza hufanyika kila wakati tunapocheza na kufurahi tukiwa peke yetu na tunapokuwa na mtu mwengine ...

Kujifunza hufanyika kila wakati **TUNAPOCHEZA** na **KUFURAH**I tukiwa peke yetu na tunapokuwa na mtu mwengine ...

- Kila siku, zunguka kwa njia yoyote unayoweza. Cheza. Rukaruka. Zungukazunguka.
- Fanya mabadiliko ya michezo ili kila mtu ajiunge nayo. Hii inaweza kuwa kubadilisha kanuni au kubadilisha harakati.
- Tunga michezo mipy na uwafundishe wengine jinsi ya kuicheza.
- Unapokuwa peke yako, unaweza kuwa na utulivu au kushughulika sana kulingana na jinsi unavyojihisi

Kujifunza hufanyika kila wakati **TUNAPODADISI** na **TUNAPOGUNDUA** zaidi kuhusu sisi wenyewe na watu wengine ...

- Jaribu kufanya kitu kipy, hata ikiwa ni vigumu kwanza.
- Jifunze kutoka kwa kila mmoja. Tafuta mtu anayeweza kukufundisha kitu unachotaka kujifunza.
- Lima chakula. Tunza mti. Rekebisha kitu. Jenga kitu. Badilisha kitu.
- Uliza maswali: Je, kwa nini hii inafanyika? Je, hii inafanyaje kazi? Je, ikiwa nitaibadilisha hii?

Kujifunza hufanyika kila wakati **TUNAPOBUNI** na **TUNAPOUNDA** kitu kwa kutumia kitu chochote kilicho karibu...

- Tumia vitu vyovyote vilivypo karibu, kama chupa zilizokwishatumi, pakiti, vijiti na matope kutengeneza vitu vingi tofauti. Kitu chochote kinaweza kutumika kusaidia ujifunze.
- Tumia mawazo yako na vitu unavyoweza kuvipata kutengeneza hadithi. Hadithi hizi zinaweza kuwa 'halisi' au za 'kubuni'.
- Fanya maigizo ya hadithi zako za kubuni. Wape wengine kile ulichokiunda. Simulia hadithi!
- Kata herufi moja moja zilizoandikwa katika pakiti zilizokwishatumi na unda maneno.

Kujifunza hufanyika kila wakati tunapojihisi **SALAMA** na **KUPENDWA** hata wakati tunapokabiliwa na matatizo ...

- Kujihisi tuko salama na wenyewe kupendwa ndio msingi wa kujifunza na ukuaji. Bila ya kujihisi salama na kupendwa inaweza kuwa ni vigumu sana kwa mtu yeyote kujifunza.
- Kumtunza mtu mwengine na kusaidiana. Kuwa mwenye huruma kwa kila mmoja, hasa wakati wa matatizo.
- Matunzo hufanyika kwa kila mtu. Watu wazima hutunza watoto, watoto hujali watu wazima, watu wazima hutunza watu wazima na watoto hujali watoto.
- Kila mtu hujifunza na kuiga tabia za watu wanaomzunguka. Onesha tabia unayotaka kuiona.